



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KATIBA NA SHERIA
WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI
(RITA)



SHERIA YA USAJILI WA WADHAMINI SURA YA 318 TOLEO LA 2002

TANGAZO KWA BODI ZA WADHAMINI WA TAASISI ZILIZOSAJILIWA
KATIKA OFISI YA KABIDHI WASII MKUU/RITA

1. KABIDHI WASII MKUU (ADMINISTRATOR GENERAL) ANAWATANGAZIA WADHAMINI WA TAASISI/ASASI ZOTE ZILIZOSAJILIWA NA OFISI YA KABIDHI WASII MKUU/RITA KUFANYA MAREJEO YA KATIBA ZA TAASISI ZAO KWA KUFANYA MAREKEBISHO ILI KUONGEZA/KUBORESHA YAFUATAYO :-
 - i. KUWEKA IBARA INAYOAINISHA CHOMBO CHA JUU CHA TAASISI HUSIKA (SUPREME AUTHORITY) KWA TAASISI ZA KIDINI;
 - ii. KUWEKA IBARA INAYOELEZEZA NAMNA YA UTATUZI WA MGOGORO/MIGOGORO INAPOTOKEA KWENYE TAASISI;
 - iii. KUWEKA IBARA INAYOONESHA MUDA WA UKOMO WA WADHAMINI KUKAA MADARAKANI;
 - iv. KUWEKA IBARA INAYOONESHA SABABU ZA MDHAMINI/WADHAMINI KUONDOKA/KUONDOLEWA MADARAKANI;
 - v. KUWEKA IBARA INAYOONESHA IDADI YA VIKAO VYA WADHAMINI KWA MWAKA NA MAJUKUMU YAKE IKIWA PAMOJA NA WAJUMBE WANAOPASWA KUHUDHURIA VIKAO HUSIKA NA AKIDI (QUORUM) KWA VIKAO;
2. AIDHA TAASISI/ASASI ZILIZOSAJILIWA OFISI YA MSAJILI WA JUMUIYA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI NA ZINAPASWA KUSAJILI BODI ZA WADHAMINI RITA LAKINI HAZIJAFANYA HIVYO ZINAPASWA KUFANYA HIVYO KWA MUJIBU WA SHERIA. VILEVILE BODI ZA WADHAMINI WA TAASISI ZA KIDINI AMBAZO HAZIKUSAJILIWA MAMBO YA NDANI ZINAELEKEZWA KUFANYA HIVYO.
3. BODI ZA WADHAMINI ZILIZOSAJILIWA RITA ZINAKUMBUSHWA KUWASILISHA MAREJESHO/ ADA YA KILA MWAKA KUZINGATIA MWEZI WALIOSAJILIWA. HATUA ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA KWA WATAKAOSHINDWA KUTEKELEZA KWA WAKATI

IZINGATIWE KWAMBA, MWISHO kuwasilisha Katiba zikiwa na marekebisho hayo ni tarehe 25 Oktoba, 2022.

IMETOLEWA hapa Dar es Salaam kwa mkono na sahihi yangu leo hii tarehe 20 Julai 2022.

Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu (RITA)
S.L.P. 9183,
DAR ES SALAAM.
Simu: 022-2924180/181
Nukushi: +022-2924182
Tovuti: www.rita.go.tz

ANGELA K. ANATORY
KABIDHI WASII MKUU/ AFISA MTENDAJI MKUU